

HALMASHAURI YA MANISPAA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI IPEPA

S.L.P 396,

SUMBAWANGA

14/12/2020.

JINA LA MWANAFUNZI

S.L.P

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPEPA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule hii ipo katika kata ya Mollo kijiji cha Ulinji Manispaa ya Sumbawanga. Ni shule ya kutwa mchanganyiko yaani wavulana na wasichana. Unatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe 06/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2021. Hatua kali zitachukuliwa dhidi yako wewe na mzazi wako kama hutaripoti kwa muda huo.

SARE

(a) WAVULANA

- sare ya shule hii ni suruali mbili, suruali moja iwe ya kaki na nyingine iwe ya kijani zishonwe vizuri, ziwe na mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma. Ukishona suruali kubwa kiuno au chembamba utarudishwa ukarekebishe ndipo upokelewe. Mashati mawili mikono mirefu, viatu vyeusi vya ngozi, soksi nyeusi, sweta la kijani, tai ya kijani na kaki na mkanda mweusi

(b) WASICHANA

- Sare ya shule hii ni sketi mbili (2), sketi moja iwe ya kaki na nyingine iwe ya kijani zishonwe vizuri. Zishonwe mshono wa marinda mawili mbele na nyuma. Ziwe ndefu kuvuka magoti na zenye vishikizo imara na zipu. Ukishona sketi hovyoy utarudishwa ukarekebishe ndipo upokelewe. Sketi isiwe na belti kubwa.
- Aje na U.P.T na cheti kinachothibitisha kutokuwa na ujauzito.
- Mashati mawili mikono mirefu, viatu vyeusi vya ngozi, soksi nyeupe na sweta lakijani pamoja na tai ya kijani au kaki

SARE YA MICHEZO

Sare ya michezo kwa shule hii ni TRAKSUTI NYEUSI yenye mistari myeupe na RABA za michezo rangi yoyote ile kwa wavulana na wasichana.

MAHITAJI YA KITAALUMA

- Aje na kiti pamoja na meza
- Aje na karatasi (Rimu) A₄ ambayo itatumika mwaka mzima
- Njoo na mzdaftari 10 (counter book Q2), mkebe, kalamu za kutosha, faili moja na kamusi ya Kiswahili-kiingereza kwa ajili ya matumizi yako katika kujifunza hapa shuleni na rula moja.

MAAGIZO MENGINE

- Tafadhari njoo na mti wa matunda utakao upanda hapa shuleni na kuutunza wewe mwenyewe. Hili ni agizo la Mkuu wa Mkoa katika suala la utunzaji wa mazingira.
- Fika na vitu vifuatavyo bila kukosa:- fagio, ndoo, jembe na fyekeo

NB. Medical form ijazwe na mganga mkuu wa Manispaa na si vinginevyo na risiti iwasilishwe
Shuleni

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu sayansi, teknolojia na ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia maagizo hayo. Utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule
- Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- Kutunza mali za umma mfano majengo ya shule viti, meza, vyoo, vioo n.k

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi, kubeli, sigara n.k
- e) Kupiga au kupigana
- f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- i) Kuoja au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo hayo nakuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
JANE FRANCISCO KANYAMA
MKUU WA SHULE

FOMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

WIZARA YA ELIMU YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI IPEPA

FOMU YA KUKUBALI/KUTOKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI IPEPA MWAKA.....

Mimi ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga kidato
cha kwanza katika shule ya sekondari Ipepa.

Nimezisoma kwa makini sheria za shule na ninaahidi kuzifuata. Vilevile nimesoma kwa uangalifu
maagizo ya kujiunga na shule na ninaahidi nitafika na vitu vyote nilivyoagizwa.

.....

SAINI YA MWANAFUNZI

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Miminikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi
..... ninakubali na kuahidi kumsaidia mwanafunzi katika masomo na
kumtimizia mahitaji yake yote ya shule kwa wakati unaotakiwa.

.....

SAINI YA MZAZI/MLEZI

NB kutotekeleza maagizo kutasababisha mwanafunzi akose masomo na mzazi/mlezi
kuchukuliwa hatua.